



Maswali na Majibu (Kuambukizwa virusi kwa kufanya mapenzi)

Q. Virusi vina ambukizwa kwa njia gani wakati wa kufanya mapenzi.?

Njia moja ya kueneza virusi ni kwa kufanya mapenzi. Virusi vina ambukizwa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine kwa kupitia maji maji ya mwili ya mwanamke na mwanamume. Virusi hutoka kwa mwili ya mtu mmoja na kuingia mwili ya mtu mwingine. Pia damu ya mwezi inaweza ambukiza virusi vya ukimwi. Mtu anaweza pata virusi vya ukimwi akifanya mapenzi na mtu mwenye virusi hivi na pia mtu anaweza kosa kupata virusi. Nilazima virusi viingie kwenye mwili na kupatana na damu na hii inaweza kosa kufanyika. Kuna njia za kuonyesha kama mtu ako kwa hatari ya kupata virusi wakati ana fanya mapenzi kama vile: ugonjwa za zinaa, njia ya kufanya mapenzi, kutumia kinga, kama mtu ana vidonda kwenye pande za siri na kadhalika.

Q. Naweza aje fanya mapenzi salama?

Kuna njia tofauti za kufanya mapenzi, kwanza kuna njia ambazo hazina hatari kama vile kubusu na kushikana, bora hakuna vidonda mkononi. Pia njia ya pili ambayo ina hatari lakini si ya kiwango ya juu ni kufanya mapenzi kwa kutumia mdomo na mwishowe ni kufanya mapenzi ambayo ina hatari ya juu kama mtu hatumi kondomu kwani mwenzake anaweza kuwa na virusi vya ukimwi. Hatari ya kupata virusi inateremka wakati mtu anatumia kondomu, ana jua hali yake na ya mpenzi wake na pia kuwa na mpenzi mmoja. Njia hizi zinateremsha hatari ya kupata virusi.

Q. Kufanya mapenzi kwakutumia mdomo ni sawa? Na ni sawa kiwango gani?

Njia hii ina hatari ya chini ikilinganishwa na kufanya mapenzi lakini hatuwezi kusema haina hatari. Virusi huambukizwa na maji maji ya mwili lakini na kama mtu ana vidonda mdomoni basi virusi vinaweza ingia kupitia hapo, pia hatari ya magonjwa ya zinaa iko juu.

Q. Naweza teremsha aje hatari ya kupata virusi wakati wa kufanya mapenzi kwa kutumia njia kama mdomo?

Kwa kutumia kondomu, hii inateremsha hatari ya kupatana na maji maji ya mwili pia ni vizuri kuhakikisha hakuna vidonda mdomoni na avizuri kutofanya mapenzi baada kusugua meno ama kula vyakula vigumu au vikali.